**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI**

**ZA MITAA SHULE YA SEKONDARI ITIGI MAJENGO**

**S.L.P 70 – ITIGI**

**NAMBA ZA SIMU:**
Mkuu wa shule: **0766187871/0782282444**
MAkamu mkuu wa shule: **0769174994**
Mwalimu wa malezi (KE): **0672552977**
Email: itigimajengoss@gmail.com

**MZAZI WA MWANAFUNZI**
**……………………………….**
**S.L.P………………**
**………………**

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA………. SHULE YA SEKONDARI ITIGI MAJENGO HALMASHAURI YA WILAYA ITIGI MKOA WA SINGIDA MWAKA……….**

## 1.0. UTANGULIZI:

Napenda kukutaarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha………. katika Shule ya Sekondari **ITIGI MAJENGO**. Hongera sana. Hii imetokana na bidii na juhudi zako ulizozionesha katika masomo yako ya kidato cha kwanza hadi cha nne.

Shule ya Sekondri Itigi Majengo ni Shule yenye Wanafunzi wa kidato cha kwanza hadi cha Sita, ni Shule ya kutwa kwa kidato cha kwanza hadi cha nne **(Wavulana na Wasichana)**. Vile vile ni Shule ya bweni kwa wanafunzi wa kidato cha tano na sita **(Wasichana).** Tunakukaribisha sana ili upate elimu bora.

Aidha, nafasi uliyopata ni ya kujivunia na unatakiwa kuitumia vema kwa manufaa yako, familia na Taifa kwa ujumla,kumbuka **"Elimu kwa Ustawi wa Jamii na Uchumi imara".** Kesho iliyo bora ni matokeo ya maandalizi yako ya sasa katika elimu bora na endelevu. Mwanzo wa muhula utaanza baada ya tangazo la Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI

Aidha, una muda mrefu wa kujiandaa, hakuna sababu ya kuchelewa kuripoti shule. Ninasisitiza mwanafunzi afike shuleni mapema bila kuchelewa,kama kuna dharura tumia namba za simu zilizotolewa hapo juu kuutaarifu Uongozi.

## 2.0. MASOMO YANAYOFUNDISHWA

- Shule ni ya mchepuo wa Sayansi tu kwa tahasusi ya **PCM** na **PCB**. Hivyo,masomo yanafundishwa ni pamoja na Physics, Chemistry, Biology, Advanced Mathematics, Basic Applied Mathematics na Historia ya Tanzania na Maadili

## 3.0. MAHALI SHULE ILIPO

- Shule ipo makao makuu ya Wilaya ya Itigi Mkoa wa Singida. Ni umbali wa kilomita moja kutoka kituo kikuu cha mabasi na ni kilomita moja na nusu kutoka makao makuu ya Wilaya. Unapopita barabara kuu kutoka Dodoma au Tabora unaweza kuona majengo ya Shule upande wa Kusini.

**4.0. OFISI UTAKAZOPOKELEWA**

- Ukifika Shuleni nenda moja kwa moja **ofisi ya mkuu wa shule** kwa ajili ya maelekezo na utaratibu wa usajili
- Muda wa usajili ni kuanzia saa **1:30 Asubuhi** hadi saa **12:00 Jioni**

**5.0. MICHANGO YA SHULE**

**5.1. MICHANGO MUHIMU YA SHULE**

| NA | AINA YA MCHANGO | KIASI |
|---|---|---|
| 1 | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 2 | Tahadhali | 5,000/= |
| 3 | Nembo ya Shule | 5,000/= |
| 4 | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**MUHIMU:**

i. Kila mwanafunzi aje na **BIMA YA AFYA**, Shule haigharamii matibabu kwa wanafunzi,hilo ni jukumu la mzazi na kwa yule ambaye hana bima aje na fedha 50,400/= kwa ajili ya bima.

ii. Fedha ya BIMA ITALIPWA Shuleni wakati wa kuripoti hivyo **FEDHA HIZO ZISIWEKWE KWENYE AKAUNTI YA SHULE**

iii. Fedha za michango muhimu (Jedwali 5.1) ya shule zilipwe kwenye akaunti ya shule
JINA LA AKAUNT: ITIGI MAJENGO SECONDARY SCHOOL CAPITATION ACCT
AKAUNTI NAMBA: 51910018065 JINA LA BENKI: NMB

iv. Tafadhali unapofanya malipo andika jina la mwanafunzi husika anayelipa mchango (michango) kwenye Bank Pay in Slip na si vinginevyo.

v. Kila mwanafunzi ahakikishe anafanya malipo yote yalivyoanishwa hapo juu.

i. **5.2**. **MAHITAJI YA TAALUMA**

i. Rimu mbili (2) A4 aina ya **Double A** (80gms) kwa mwaka
ii. Dissecting kit kwa wanafunzi wote
iii. Jalada au file jipya (spring file)
iv. Scientific calculator – function 991
v. Mdaftari yanayotosheleza matumizi ya mwanafunzi kwa mwaka mzima (Counter Books kuanzia Quire 3)
vi. Stop watch kwa wanafunzi wote
vii. Unashauriwa kuja na vitabu vinavyoendana na tahasusi (Combination) yako

**Yafuatayo ni mapendekezo ya aina za vitabu vinavyotumika kwa kidato cha tano na sita**

| SOMO | BIOLOGY | PHYSICS | CHEMISTRY | ADV.MATH'S | B.MATH'S | HTM |
|---|---|---|---|---|---|---|
| AINA YA VITABU | -Biological Science<br>-Comprehensive Biology<br>-Understanding Biology<br>-CHAND | -Principles of Physics by Nelkon 5th Edition<br><br>-CHAND Class XI and XII<br>-ABC Modern Physics 1, 2 | -CHAND XI and XII<br><br>-A Level Chemistry Ramsden 4th Edition<br><br>-Conceptual Chemistry | -CHAND Class XI & XII<br><br>-Pure Mathematics I & ii by Bck House<br><br>-Advanced Mathematics by Tranter | -Applied Mathematics by CHAND S.<br><br>-Applied Mathematics by Dr. J.S. Bindra | |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | -Roger Muncaster | -Organic Chemistry Part I & II<br><br>-Inorganic Chemistry Part I & II<br><br>-Soil Chemistry<br><br>-Physical Chemistry foe A-Level | | | |

**5.3 MAHITAJI YA VIFAA VYA USAFI, MALAZI, NA CHAKULA**

i. Squizer 1 (PCB)
ii. Mfagio 1 wa sakafu (soft bloom) (PCM)
iii. Jembe 1 lenye mpini (PCB)
iv. Sanduku 1 la chuma
v. Sabuni ya chooni aina ya **Aro** (PCB, PCM)
vi. Fyekeo (kwanja) 1 (PCB, PCM)
vii. Mfagio mgumu 1 (hard bloom) (PCM)
viii. Mfagio 1 wa chelewa(PCB)
ix. Panga 1 (PCM)
x. Ndoo 2 ndogo zenye mifuniko na galoni ya kutunzia maji ya kunywa xi. Kanda mbili pea 1 kwa ajili ya kuogea
xi. Godoro 1 (ft 2.5 x 6)
xii. Shuka 2 rangi ya light blue na foronya rangi light blue
xiii. Chandarua kimoja pembe 4
xiv. Blanket 1
xv. Vyombo vya chakula: kijiko, kikombe na sahani (visiwe vya plastic)

**Angalizo:** Mafuta ya kubadilisha rangi ya ngozi, mafyta yenye hrufu kali (perfume, body spray) **HAYARUHUSIWI**

**5.4. SARE YA SHULE NA NGUO ZA MICHEZO**

a. Sare ya shule ni sketi 2 za rangi ya KAROTI mshono wa kawaida. Rinda kubwa 2 moja mbele na jengine nyuma halafu pembeni marinda madogo 3 kila upande. Iwe ndefu kawaida ifunike magoti mpaka mpaka kwenye kifumdo cha mguu.
b. Mashati 2 ya mikono mirefu rangi ya Nyeupe c) S o c k s fupi Nyeupe jozi 2
c. Sweta1 la mikono mirefu rangi ya Kijivu lenye shingo ya "V"
d. Wanafunzi wanaovaa Hijabu au Juba iwe na rangi Nyeupe na ishonwe na kuvaliwa kwa kuzingatia matakwa ya vazi lenyewe.
e. Viatu vyeusi vya ngozi jozi 2 vya kufunga kwa kamba. Viwe na kisigino kifupi
f. Nguo za kushindia (shamba dress) sketi 2 zenye mshono ufanane na sketi za shule, rangi ya dark blue (Kitambaa cha suti)
g. Nguo za nyumbani haziruhusiwi kabisa isipokuwa mwanafunzi aje na kanga/vitenge jozi 1, tu atatumia wakati wa kuoga.
h. T-shit 2 za kushindia rangi ya Kijivu mojawapo iwe ya michezo yenye rangi ya light blu
i. Track suit kwa ajili ya michezo pea 1 rangi light blue l) Raba kwa ajili ya michezo jozi 1
j. m) Stocking za michezo jozi 2 rangi nyeusi zenye ufito mweupe juu.

## 6.0. TAALUMA

Shule hii inajali sana taaluma bora kwa wanafunzi wote hivyo, mwanafunzi aliyechaguliwa kujiunga katika shule hii ana bahati na anatakiwa kusoma kwa bidii zote na kuachana na tabia zitakazomuathiri kimasomo ili aweze kafaulu vizuri masomo yake. Uongozi wa Shule hautavumilia hata kidogo wanafunzi wanaotoroka ratiba za darasani. Utaratibu wa wiki nzima **(school weekly routine)** utatolewa na kumpa fursa mwanafunzi kufuata kwa ukamilifu ratiba ya Shule. Aidha, kutokufanya mtihani au jaribio ni kosa linaloweza kumsababishia mwanafunzi kupoteza nafasi yake ya kuwa shuleni.

## 7.0. HESHIMA, ADABU NA UTII

### 7.1. Heshima, Adabu na Utii

Mwanafunzi aliyepata nafasi ya kujiunga na Shule hii hana budi kuwa na adabu, utii na heshima kwa walimu wake, watumishi wengine, wanafunzi wenzake na jamii kwa ujumla. Mwanafunzi atakayebanika kutokuwa na tabia njema au kuwa jeuri ATAFUKUZWA SHULE MARA MOJA. Aidha, mzazi anatakiwa amwonye mwane na kumtahadharisha na tabia za kutofuata sharia za Shule.

### 7.2. Sheria za Shule

Sheria zifuatazo zinatakiwa kuzingatiwa na mwanafunzi siku zote awapo Shuleni na mahala pengine popote nje ya Shule:

1. Mwanafunzi lazima awe na utii na heshima kwa walimu, viongozi, watu wazima, wageni na kati yao wenyewe.
2. Ni wajibu wa mwanafunzi kutunza mali za Shule
3. Wanafunzi hawaruhusiwi kuvuta sigara,kunywa pombe,kutumia dawa za kulevya na wizi
4. Wanafunzi hawaruhusiwi kufika nyumbani kwa walimu au nje ya mipaka ya shule bila ruhusa
5. Ni marufuku kuingia nyumba za starehe kama vile bar, dansini (ukumbi wa disco) na nyumba za kulala wageni (guest house)
6. Ni wajibu wa wanafunzi kuona kuwa viwanja vya Shule, madarasa na vyumba vingine vimewekwa katika hali ya usafi.
7. Matusi ya kusema au kuandika na ugomvi haviruhusiwi
8. Mwanafunzi lazima ahudhurie vipindi vya dini yake kila siku
9. Ni mwiko kwa mwanafunzi kujiunga na vikundi vyenye tabia mbaya shuleni au nje ya shule
10. Kila mwanafunzi anapaswa kuwahi Assembly ground kila inapofika saa 6:30 asubuhi kwa ajili ya kuhesabu namba na kuendelea na ratiba ya shule kama ilivyoainishwa na utawala
11. Ni wajibu wa kila mwanafunzi kushiriki kikamilifu katika mipango yote ya shule ya elimu ya kujitegemea. Uvivu au utoro ni makosa makubwa
12. Ni marufuku kupokea wageni. Wageni wote wapitie kwa mkuu wa shule
13. Ni marufuku kujiunganisshia au kuunganisha umeme katika maeneo yoyote ya shule
14. Ni marufu kuzagaa nje ya madarasa wakati wa vipindi
15. Mwanafunzi haruhusiwi kujipikia au kuchemsha chochote awapo shuleni isipokuwa kwa ruhusa maalumu kutoka utawala
16. Mwanafunzi haruhusiwi kuvaa nguo au viatu ambavyo siyo sare ya shule ndani na nje ya shule

17. Ni marufuku kwa mwanafunzi kuonekana au kulala bwenini wakati vipindi vinaendelea au wakati wa maandalizi ya usiku **Night preparation**
18. Mwanafunzi haruhusiwi kugomea adhabu
19. Mwanafunzi hatakiwi kuchelewa kuripoti shule akitoka likizo. Endapo atafanya hivyo atarudishwa nyumbani kumfuata mzazi wake ili aeleze sababu za kuchelewa kufika shuleni kwa wakati. Kama sababu za mzazi hazitajitoshereza mwanafunzi atapewa adhabu stahikikwa kuzingatia maoni ya ofisi ya nidhamu.
20. Simu za mkononi, charger, battarery na line ya simu haziruhusiwi kabisa shuleni;mwanafunzi akikamatwa na simu shuleni atafukuzwa shule mara moja.

**Makosa mengine yanayoweza kusababisha mwanafunzi kufukuzwa shule ni pamoja na:**

- Wizi
- Uasherati, ubakaji, usagaji
- Ulevi
- Kupigana au kupiga
- Kugomea adhabu, kuchochea na kuongoza au kuvuruga Amani na usalama w shule au watu
- Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
- Kudharau bendera ya Taifa
- Kuolewa
- Kupata mimba, kushiriki au kutoa mimba

## 8.0. VIAMBATANISHO NA FOMU MUHIMU

1. Fomu ya uchunguzi wa afya **(Medical Examination form)** ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali yoyote ya serikali
2. Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi – mkataba wa kutoshiriki katika mgomo, fujo na makosa ya jinai.
3. Fomu ya kukiri kukubaliana na sharia, kanuni, miongozo na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule
4. Picha 4 za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu

**MUHIMU:**

- ❖ Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika kwa mwanafunzi mmoja tu.
- ❖ Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalumu toka kwa mkuu wa shule. (msiba au ugonjwa)

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI**
**ZA MITAA SHULE YA SEKONDARI ITIGI MAJENGO**
**S.L.P 70 – ITIGI**

## FOMU YA KUKIRI KUKUBALIANA NA SHERIA, KANUNI, MICHANGO NA MAELEKEZO MENGINE YATAKAYOTOLEWA NA SHULE

Mimi……………………………….. **(jina la mwanafunzi)** nimesoma,nimeelewa na ninakubaliana nan a maagizo yote yanayotolewa katika barua ya maelekezo niliyopewa na shule hii. Ninaahidi kwamba nitafuata sharia zote za shule na kutimiza wajibu wangu katika muda wote nitakapokuwa mwanafunzi wa shule hii.

Sitajihusisha na mgomo wala kuchochea mgomo, makosa ya jinai au kujihusisha na vitendo vinavyoweza kuhatarisha Amani ya shule hii. Kwa jinsi hiyo,uongozi wa shule uchukuwe hatua ya kuniondoa au kunisimamisha masomo au adhabu yoyote pale nitakapokwenda kinyume na maagizo, kanuni,au sharia za shule. Ninaahidi pia kuwa nitakuwa mwanafunzi mwema wakati wote niwapo ndani au nje ya shule.

Saini ya mwanafunzi……………….

Jina la mwanafunzi……………………………

Tarehe…………………………..

Saini ya mzazi au mlezi………………………………..

Jina la mzazi au mlezi……………………………….

Namba ya simu ya mzazi au mlezi………………….

Tarehe………………………..

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI**
**ZA MITAA SHULE YA SEKONDARI ITIGI MAJENGO**
**S.L.P 70 – ITIGI**

**TAARIFA MUHIMU KWA MWANAFUNZI**

1. Jina lako……………………………….. (jina hili ni lazima lifanane na jina linalosomeka kidato cha nne)

2. **Baba**
   i. Jina la baba yako………………………………
   ii. Yu-hai NDIYO ( ) HAPANA ( ) weka alama ya vema panapohusika
   iii. Kama amefariki taja ni lini………………….
   iv. Kama yu-hai anuani yake ni: …………… namba ya simu………………….
   v. Kazi na cheo chake………………………….
   vi. Dini ya baba yako……………………………..

3. **Mama**
   i. Jina la mama yako………………………………
   ii. Yu-hai NDIYO ( ) HAPANA ( ) weka alama ya vema panapohusika
   iii. Kama amefariki taja ni lini………………….
   iv. Kama yu-hai anuani yake ni: …………… namba ya simu………………….
   v. Kazi na cheo chake………………………….
   vi. Dini ya mama yako……………………………..

4. **Mlezi**
   i. Unaye mlezi? (mlezi ni mtu asiye mzazi wako) anayekutunza na kukuhudumia kwa chakula, malazi, n.k
   NDIYO ( ) HAPANA ( ) weka alama ya vema panapohusika
   ii. Kama ni NDIYO
      a) Jina la mlezi huyo ni …………………………..
      b) Uhusiano wako na mlezi (mjomba, rafiki, kaka, shangazi n.k)
      c) Anuani ya mlezi wako…………………….
      d) Kazi ya mlezi wako………………………….
      e) Namba ya simu ya mlezi wako…………………

5. Jina la mtu anayepelekewa ripoti zako za shule kama si baba/mama au mlezi wako ni:
   Jina…………………………………….
   Anuani yake…………………………
   Namba yake ya simu……………………..

   **MUHIMU:**
   Mwanafunzi atalazimika kuja na cheti cha matokeo ya mtihani wa kidato cha nne (result slip), nakala ya cheti cha kuzaliwa na kadi ya NIDA kama anayo

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA SHULE YA SEKONDARI ITIGI MAJENGO**

**S.L.P 70 – ITIGI**

**FOMU NA PICHA ZA WAZAZI NA NDUGU WA KARIBU NA MWANAFUNZI WANAOWEZA KUMTEMBELEA MWANAFUNZI SHULENI PAMOJA NA NAMBA ZAO ZA SIMU.**

| NA. | JINA LA NDUGU | MAHUSIANO | NAMBA YA SIMU | PICHA |
|---|---|---|---|---|
| 1. | | | | |
| 2. | | | | |
| 3. | | | | |
| 4. | | | | |

**PRIME MINISTER'S OFFICE**
**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**
**ITIGI MAJENGO SECONDARY SCHOOL**
**P.O. BOX 70 – ITIGI**

**ITIGI MAJENGO SECONDARY SCHOOL,**
**P.O. BOX 70,**
**ITIGI**
**DATE: ……………….**

To the medical officer,
………………………………………..
Dear sir/madam

REF: REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION:

Please examine Miss

……………………………………………………………………… as to her fitness as a full-time student of this school may I kindly request you to fill in the particulars given in the form here under.
(Yours Sincerely)
………………………………………………………….
The Headmaster
………………………………………………………….

TO BE COMPLETED BY THE MEDICAL OFFICER

1. Blood count (white blood cell) ………………………………………………………………..
2. Stool examination ………………………………………………………………………………..
3. Urine examination………………………………………………………………………………..
4. Gestation ……………………………………………………………………………………………
5. Venereal diseases …………………………………………………………………………………
6. T. B. test …………………………………………………………………………………………….
7. E. N. T. problem …………………………………………………………………………………
8. Defects of (a) The left and right eye ………………………………………………………………
   (b) The chest ……………………………………………………………………………….
9. Does she has any CHRONIC disease eg. Epilepsy cell, Anemia, Athma etc.

……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………

I have examined Miss ………………………………………………………………… And certify that she is physically fit to persue studies as stated above

……………………………………………………………………………………………………

Name and signature of the medical officer

Date …………………………………….

Designation ……………………………..